**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA**

# BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2025/26 KWA LUGHA RAHISI TOLEO LA MWANANCHI

# Yaliyomo

1. Utangulizi ........................................................................... 1

2. Mapato na Matumizi ........................................................................... 3

2.1 Je, Serikali inatarajia kukusanya mapato kutoka vyanzo vipi? 3

2.2 Je, matumizi ya Serikali ni yapi? ........................................... 4


3. Maboresho ya Mfumo wa Kodi, Ada, Tozo ................... 8

## 1. Utangulizi

**Bajeti ya Serikali** ni mpango wa kifedha unaoandaliwa kwa kipindi cha mwaka mmoja unaoonesha mapato na matumizi yanayotarajiwa. Kupitia bajeti, Serikali huorodhesha vyanzo vya mapato vya ndani kama kodi na vyanzo vya mapato vya nje ikiwemo misaada na mikopo. Vilevile, Serikali hupanga kutumia mapato yatakayokusanywa kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ili kugharamia utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi ikiwemo elimu, afya, maji na miundombinu ya barabara.

Nchini Tanzania, mwaka wa fedha au bajeti ya Serikali huanza kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Julai hadi 30 Juni. Kwa mwaka 2025/26 (Julai 2025 – Juni 2026) dhima kuu ya Bajeti kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni "Mageuzi Jumuishi ya Uchumi kupitia Uimarishaji wa Ukusanyaji Mapato ya Ndani, Uwekezaji wa Kimkakati wenye Kuzalisha Fursa za Ajira na Uboreshaji wa Hali ya Maisha ya Wananchi".

**Bajeti ya Serikali Toleo la Mwananchi** ni muhtasari wa Bajeti ya Serikali uliotayarishwa kwa lugha rahisi ili kuwawezesha wananchi kuelewa kwa urahisi jinsi Serikali itakavyokusanya mapato na kutumia fedha za umma. Kitabu hiki husaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa kurahisisha upatikanaji wa taarifa za bajeti.



## Malengo ya Kiuchumi

**Kuongeza Ukuaji wa Pato la Taifa**
Kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa hadi 6.0% ifikapo 2025

**Kudhibiti Mfumuko wa Bei**
Kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki kati ya 3.0-5.0%


**Kuongeza Mapato ya Ndani**
Kuongeza mapato ya ndani hadi 16.7% ya Pato la Taifa

**Kuongeza Mapato ya Kodi**
Kuongeza mapato ya kodi hadi 13.3% ya Pato la Taifa

**Kupunguza Nakisi ya Bajeti**
Kupunguza nakisi ya bajeti hadi 3.0% ya Pato la Taifa

**Kudumisha Akiba ya Fedha za Kigeni**
Kuhakikisha akiba ya fedha za kigeni inatosha kwa miezi minne ya uagizaji

## Misingi ya Uchumi kwa 2025/26



**Ushiriki wa Sekta Binafsi**
Kuongeza uwekezaji na biashara kupitia sekta binafsi

**Ustahimilivu wa Majanga**
Kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili

**Utulivu wa Uchumi wa Dunia**
Kuimarisha utulivu wa uchumi wa dunia na masoko

**Usalama wa Chakula**
Kuimarisha upatikanaji na usalama wa chakula nchini

**Amani na Usalama**
Kuhakikisha amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na kikanda

## Vipaumbele vya Bajeti

**Kukamilisha Miradi ya Kimkakati**
Kukamilisha miradi ya kimkakati na kielelezo.

**Kuimarisha Sekta za Uzalishaji**
Kuimarisha sekta za uzalishaji kwa uchumi.


**Kuimarisha Rasilimali Watu**
Kuimarisha rasilimali watu katika huduma za jamii.

**Kuboresha Mazingira ya Biashara**
Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

## 2. Mapato na Matumizi

### 2.1 Je, Serikali inatarajia kukusanya mapato kutoka vyanzo vipi?

Serikali inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi trilioni 56.49 kutoka katika vyanzo mbalimbali.






## 2.2 Je, matumizi ya Serikali ni yapi?

Katika mwaka 2025/26 Serikali inatarajia kutumia shilingi trilioni 56.49 kugharamia mahitaji mbalimbali ikiwemo:

(i) Miradi na programu za maendeleo shilingi trilioni 18.92;


(ii) Mishahara ya watumishi shilingi trilioni 13.17;

(iii) Uendeshaji wa shughuli za Serikali katika kutoa huduma kwa wananchi shilingi trilioni 10.19;

(iv) Malipo ya mtaji shilingi trilioni 7.72; na

(v) Malipo ya riba shilingi trilioni 6.49.

### Mikakati ya Usimamizi wa Fedha za Umma




### Mwelekeo wa Matumizi ya Fedha za Umma katika Mamlaka Za Serikali za Mitaa

| Eneo | Ugawaji (Shilingi) | Maelezo |
|---|---|---|
| Mishahara ya Wafanyakazi | Trilioni 6.10 | Kugharamia mishahara ya watumishi. |
| Elimu Bila Ada | Bilioni 510.96 | Kuwezesha elimu ya msingi na sekondari bila ada. |
| Usimamizi wa Mitihani ya Kitaifa | Bilioni 273.2 | Usimamizi wa mitihani ya kitaifa. |
| Mikopo (Wanawake, Vijana, Watu Wenye Ulemavu) | Bilioni 123.4 | Kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. |
| Ujenzi wa Masoko | Bilioni 122.91 | Kujenga masoko 21, ikiwa ni pamoja na masoko ya samaki na mazao. |
| Mradi wa TASAF | Bilioni 84.23 | Kuziwezesha kaya masikini. |
| Ujenzi wa Majengo ya Serikali | Bilioni 78.98 | Kujenga majengo ya utawala, nyumba za wakurugenzi na wakuu wa idara |
| Miradi ya Mapato ya Serikali za Mitaa | Bilioni 44.85 | Kutekeleza miradi ya kuongeza mapato ya ndani. |
| Ujenzi/Karakati wa Hospitali | Bilioni 35.7 | Kujenga na kukarabati hospitali za halmashauri. |
| Ununuzi wa Vifaa vya Tiba | Bilioni 33.8 | Kununua vifaa vya tiba kwa vituo vya afya, zahanati na hospitali. |
| Kumaliza maboma | Bilioni 21.83 | Kumaliza maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. |


**Mnyumbuliko wa Matumizi ya Serikali katika Mfumo wa Kiuchumi**

| Kategoria | Maelezo | Kiasi (Shilingi Bilioni) |
|---|---|---|
| **Mishahara na stahiki za watumishi** | Malipo kwa watumishi | 9,172.00 |
| **Gharama za bidhaa na huduma** | Gharama za bidhaa na huduma zinatotumiwa na Serikali | 5,576.10 |
| **Malipo ya riba** | Gharama za malipo ya riba | 6,493.70 |
| **Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji** | Fedha zinazoelekezwa kwa baadhi ya taasisi za uwekezaji za Serikali. | 112.60 |
| **Ruzuku na michango** | Fedha zinazoelekezwa kwa mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za mitaa. | 22,052.90 |
| **Mafao na misaada ya kijamii** | Misaada ya kijamii pamoja na malipo ya fidia na misaada inayohusiana na masuala ya kiutumishi. | 1,001.90 |
| **Gharama nyingine** | Matumizi mengine yakijumuisha programu ya TASAF . | 2,043.80 |
| **Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha** | Uwekezaji katika mali kama vile majengo. | 2,322.00 |
| **Malipo ya mtaji kwa deni** | Malipo ya mtaji kwa deni | 7,715.2 |

## Mgawanyo wa Bajeti ya Serikali Kisekta



## Dondoo za Matumizi ya Sekta Elimu



**Utekelezaji wa Mtaala**

Kuanzisha mtaala wa Elimu ya Amali katika ngazi zote za elimu

**Ufadhili wa Mikopo ya Wanafunzi**

Kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati


**Elimu ya Ufundi na Mafunzo**

Kuwekeza katika programu za ufundi na mafunzo ya ufundi stadi

## Dondoo za Matumizi ya Sekta ya Afya

**Miundombinu ya Afya**

Kuboresha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na miundombinu katika hospitali, vituo vya afya na zahanati




**Huduma za Afya**

Kuboresha huduma za afya ya uzazi, mama na toto, chanjo na Programu ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamie


**Upatikanaji wa Dawa**

Kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini na vifaa


## Dondoo za Matumizi ya Sekta ya ya Kinga ya Jamiii





## Dondoo za Matumizi ya Sekta ya Ulinzi, Usalama na Utii wa Sheria




## Dondoo za Matumizi ya Sekta ya Maendeleo ya Uchumi






## 3. Maboresho ya Mfumo wa Kodi, Ada, Tozo

Serikali imefanya maboresho mbalimbali katika mifumo ya kodi, ada na tozo kupitia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2025. Maboresho yaliyofanyika yanalenga kuongeza wigo wa kodi, kulinda viwanda vya ndani, kutoa nafuu kwa wakulima, kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji. Baadhi ya maboresho hayo ni kama ifuatavyo:

| Na | Sheria | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148** | Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani katika maeneo mbalimbali ikiwemo:<br>(i) Viuatilifu kwa lengo la kuwapa unafuu wakulima kupata dawa za kuua wadudu mashambani;<br>(i) mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini ili kuleta unafuu wa bei ya mafuta ya kula nchini; na<br>(ii) gesi asilia inayouzwa kwenye vituo vya kushindilia gesi kwenye magari kwa lengo la kuvutia wawekezaji, kupunguza utegemezi wa mafuta na uzalishaji wa hewa ya ukaa.<br><br>Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa:<br>(i) kiwango cha asilimia 0 kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba na viwanda vinavyotengeneza nguo nchini; na<br>(ii) mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu ili kuimarisha viwanda vya ndani na kuleta unafuu kwa wakulima.<br><br>Kutoza kiwango cha punguzo la kodi ya ongezeko la thamani cha asilimia 16 badala ya asilimia 18 kwenye ununuzi wa bidhaa pale ambapo malipo yake yatafanyika kwa njia ya mtandao. |

| Na | Sheria | Maelezo |
| --- | --- | --- |
| 2 | **Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332** | (i) Kutoza kodi ya mapato kwa kiwango cha asilimia 3.5 kwenye mapato yanayotokana na uuzaji wa mazao ya misitu;<br>(ii) Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye malipo ya kamisheni inayotokana na matangazo ya michezo ya kubahatisha; na<br>(iii) Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo yanayotokana na ununuzi wa chumvi ghafi kwa wamiliki wa leseni ya uchimbaji mdogo wa madini au wachimbaji wadogo wa madini |
| 3 | **Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147** | (i) Kufuta ada ya leseni ya kiasi cha shilingi 300,000 inayotozwa kwa wazalishaji na waingizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa ili kuwapa unafuu wazalishaji na waingizaji wa bidhaa hizo nchini; na<br>(ii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 30 kwenye vifaa vya sigara za kielektroniki ili kupunguza athari zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo. |
| 4 | **Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290** | (i) Kupunguza tozo ya ushuru wa huduma (service levy) kutoka utaratibu wa sasa wa kutoza kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya pato ghafi kwenda kiwango mfuto cha asilimia 0.25 ya pato ghafi;<br>(ii) Kupunguza kiwango cha ada ya ushuru wa hoteli (hotel levy) kutoka asilimia 10 hadi asilimia 2; na<br>(iii) Kufuta ada za upakiaji (loading) na upakuaji (offloading) zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusiana na usafirishaji wa mizigo |
| 5 | **Kanuni za Sheria ya Usalama Barabarani za mwaka 2024** | (i) Kupunguza ada ya usajili wa pikipiki za biashara kutoka shilingi 340,000 hadi shilingi 170,000 kwa miaka mitatu; na<br>(ii) Kupunguza ada ya leseni ya uendeshaji wa pikipiki, bajaji na guta kutoka shilingi 70,000 hadi shilingi 30,000. |
| 6 | **Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004** | (i) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotumia mafuta ya petroli, dizeli na gesi yanayoagizwa kwa ajili ya mradi wa usafiri wa haraka;<br>(ii) Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kutoka asilimia 35 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni za maliwato (toilet soap); na<br>(iii) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka kiwango cha asilimia 50 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye vitenge. |
| 7 | Serikali imeanzisha vyanzo vya mapato kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya Ukimwi na kugharamia Bima ya Afya kwa wote. Vyanzo hivi ni pamoja na: kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vya kilevi vinavyozalishwa na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi; kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki kutoka asilimia 17 hadi asilimia 17.5; kutoza kiwango cha asilimia 0.1 kwenye thamani ya soko ya madini; na kutoza kiasi cha shilingi 10 kwa kila lita ya mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa. | |

**Jedwali Na. 1: Mgawanyo wa Bajeti ya Serikali Kisekta**

**Shilingi Milioni**

| SEKTA | Kiasi |
|---|---|
| **1 - Elimu** | **7,394,357.49** |
| 1.1 - Elimu Msingi | 4,940,964.44 |
| 1.2 - Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 478,717.52 |
| 1.3 - Elimu ya Juu | 1,719,267.89 |
| 1.4 - Sayansi, Teknolojia na Ubunifu | 90,618.60 |
| 1.5 - Huduma za Utawala | 164,789.04 |
| **2 - Afya** | **3,104,925.58** |
| 2.1 - Huduma za Tiba | 1,405,182.64 |
| 2.2 - Huduma za Kinga | 465,726.88 |
| 2.3 - Zahanati | 50,823.43 |
| 2.4 - Vituo vya Afya | 69,456.56 |
| 2.5 - Hospitali za Wilaya | 980,437.19 |
| 2.6 - Huduma za Utawala | 133,298.87 |
| **3 - Huduma za Utawala na Deni la Serikali** | **16,222,731.65** |
| 3.1 - Utawala na Bunge | 6,411,475.19 |
| 3.2 - Usimamizi wa mapato na Matumizi | 2,977,414.24 |
| 3.3 - Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa | 340,126.79 |
| 3.4 - Deni la Serikali (Malipo ya Riba) | 6,493,715.43 |
| **4 - Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama** | **6,377,300.05** |
| 4.1 - Ulinzi | 3,642,694.38 |
| 4.2 - Usalama wa Umma | 2,046,063.01 |
| 4.3 - Mahakama | 688,542.67 |
| **5 - Maendeleo ya Uchumi** | **10,696,674.21** |
| 5.1 - Kilimo | 1,927,136.96 |
| 5.2 - Madini | 224,961.50 |
| 5.3 - Nishati | 1,965,660.67 |
| 5.4 - Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano | 5,986,972.27 |
| 5.5 - Maliasili, Utalii na Mazingira | 314,125.87 |
| 5.6 - Viwanda | 135,519.01 |
| 5.7 - Biashara | 103,850.87 |
| 5.8 - Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi | 38,447.06 |
| **6 - Hifadhi ya Jamii** | **3,183,504.48** |
| 6.1 - Wazee, Watoto na Watu wenye Ulemavu | 72,593.68 |
| 6.2 - Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | 2,659,321.33 |
| 6.3 - Mfuko wa Bima wa Afya | 451,589.47 |
| **7 - Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii** | **1,795,499.68** |
| 7.1 - Maji | 912,459.17 |
| 7.2 - Ardhi, Nyumba na Makazi ya Watu | 166,857.22 |
| 7.3 - Maendeleo ya Jamii | 196,547.03 |
| 7.4 - Habari, Michezo na Utamaduni | 519,636.26 |
| **Jumla ya Sekta** | **48,774,993.13** |
| | |
| **Deni la Serilaki (Malipo ya Mtaji)** | **7,715,263.08** |
| | |
| **Jumla Kuu** | **56,490,256.21** |

Chanzo: Wizara ya Fedha

**NYARAKA REJEA ZA BAJETI**

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka zinazochapishwa na Serikali na kutumika kama chanzo cha taarifa za kuandaa bajeti:

a) Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (TDV 2025) pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26;
b) Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi ya Mwaka 2020;
c) Hotuba ya Bajeti za Mawaziri 2025/26;
d) Hotuba ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2025/26;
e) Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2025/26;
f) Sheria ya Fedha ya Mwaka 2025;
g) Sheria ya Matumizi ya mwaka 2025;
h) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2025/26 (Juzuu Na. I – hadi IV).

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo ya nyuma ya vijitabu vya Bajeti Toleo la Mwananchi, uneweza kutembelea tovuti ya:

- Wizara ya Fedha (www.mof.go.tz)
- Tume ya Taifa ya Mipango (www.planning.go.tz)
- Bunge la Tanzania (www.parliament.go.tz)